**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2024**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu………………**

**Mkuu wa Shule: 0767175810**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0754863635**

**Matron:0621108178**

**Shule ya Sekondari ya Wasichana Ifunda**

**S.L.P. 7,**

**Tarehe: 02/04/2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA IFUNDA HALMASHAURI YA WILAYA IRINGA MKOA WA IRINGA MWAKA WA MASOMO 2024/2025.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024/2025 na atasoma kati ya tahasusi zifuatazo; PCB,PCM,PGM,CBG,EGM,HGE,HGK na HKL

Shule ya Sekondari ya Wasichana Ifunda ipo Kijiji cha Ifunda ,umbali wa Kilometa 43 Kusini mwa Mji wa Iringa Manispaa. Usafiri wa basi kutoka mjini Iringa unapatikana katika kituo kikuu cha cha mabasi cha zamani Nauli ni Shilingi 2000 na kutoka kibao cha Sekondari Ifunda kwa pikipiki Shilingi 1000. Kwa wale watakao tokea mikoa ya kusini Ruvuma, Njombe,Mbeya, Rukwa na Songwe washuke Ifunda kibao cha Sekondari na kwa wale wataotokea kanda ya Mashariki, kaskazini, magharibi na kanda ya Ziwa wapande magari ya Mbeya, Ruvuma na Njombe ili washuke Ifunda kibao cha Sekondari.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 08/07/2024, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 06/07/2024 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 14/07/2024

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1.Sare za Shule

i.Sare ya shule hii ni sketi mbili rangi ya brauni ya kuiva (Kitambaa kizito cha suti) zenye linda box katikati iwe ndefu mpaka miguuni. Printi picha ya rangi uione vizuri kwa changamoto yoyote wasiliana nasi kupitia namba hizo hapo juu.



ii.Mashati meupe ya mikono mirefu mawili (02) au zaidi.

iii.Rangi ya Hijab (kijuba)/mtandio mweupe usio na urembo wowote ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.

iv.Sare ya Michezo ni raba nyeupe, na jezi kama ifuatavyo;

a). PCB– Chelsea(bluu), (b) CBG – Juventus(pundamilia), (c) PCM – Man city(bluu bahari),(d).PGM–Bayan Munichi(nyekundu),(f).EGM –liverpool (nyekundu), (g).HGE – Real Madrid (nyeupe), (h).HGK –Arsenal (nyekundu), (i).HKL – Manchester (nyekundu)

v.Viatu vya shule ni vyeusi jozi mbili vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi na visiwe na urembo wowote.

vi.Soksi ndefu jozi tatu nyeupe zisizo na urembo wowote.

vii.Sweta 2 rangi ya kijani jeshi printi picha ya rangi uione vizuri



viii.Nguo za kushindia (*shamba dress*) sketi mbili rangi ya orange za kitambaa kizito cha suti zenye linda box katikati. Printi picha ya rangi uone



ix.Tai mbili rangi ya brown iliyoiva
x.Tisheti (T-shirt) mbili nzito nyeupe isiyo na maandishi zenye kora
xi. Pullnck nyeupe tatu au zaidi kwa ajili ya kujinga na baridi
xii.Truck suit rangi nyeusi yenye mistari myeupe pembeni na isiyo na kofia.

**2.2.Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i.Madaftari madogo(Msomi) 12 na counter book Q3 12 au zaidi na graph pad 1.
**ii.Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii.Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatanishwa* uk. 10-11)
iv.Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma baiolojia(Biology( na Koti jeupe (Lab coat) kwa wanafunzi wote wa sayansi CBG, PCB, PCM na PGM



Koti jeupe (Lab coat).

v.Scientific Calculator;
vi. Godoro dogo la futi 21/2 x 6
vii.Mashuka Jozi 2 rangi ya pink, blanket zito 1, mto na foronya rangi ya pink 2, chandarua nyeupe1.
viii.Nguo za ndani za kutosha na sanduku la chuma (tranka).
ix.Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x.Ndoo 2 lita Kumi moja na lita 20 moja zenye mifuniko,kandambili na kanga/kitenge
xi. a) HGK na HKL waje na Kwanja 1, jembe 1, mfagio mgumu (hard bloom)1 na chelewa1
b). EGM na HGE waje na mifagio laini (soft bloom) 1,mopa ya ndoo 1,kwanja 1, jembe 1 na chelewa 1
c). CBG,PCB na PCM waje na reki 1, mopa/squeezer 1,brush ya kusugulia sink la choo na kikopo chake 1, jembe 1,kwanja 1 na chelewa 1.
d). Mchepuo wa PGM waje jembe 1, chepe 1, kwanja 1 na chelewa 1

## 2.3.Michango mbalimbali

### a) Shule za Bweni

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Michango yote itumwe kupitia akaunti namba NMB 60501100110**
**JINA LA AKAUNTI, IFUNDA SECONDARY SCHOOL REVENUE COL**

## 3.Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i.Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii.Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii.Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv.Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v.Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vii.Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
viii.Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
ix.Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
x.Kutunza mali za shule;
xi.Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xii.Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

iWizi;
ii.Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii.Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv.Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v.Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi.Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii.Kufuga ndevu;
viii.Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix.Uvutaji wa sigara;
x.Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi.Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii.Kusababisha mimba;
xiii.Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv.Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv.Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi.Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii.Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii.Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4.Viambatisho na Fomu Muhimu**

i.Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii.Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii.Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv.Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.
v. Results slip ya kidato cha nne
vi. Cheti cha kuzaliwa

**5**.Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ……………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule: BLANDINA D. NKONDOLA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule: 0767175810**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0754863635**
- **Mwandamizi Taaluma: 0769238114**
- **Mwandamizi Malezi: 0621108178**

**OFISIYA RAIS TAMISEMI HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA IFUNDA**
**FOMU YA KUKUBALI NAFASI.**

TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI (Ijazwe na mwanafunzi mwenyewe) Jina kamili (kama kwenye results slip) …………………………………….. Tarehe kuzaliwa ………………. Kabila ………………….. Dini na dhehebu ………………. Comb niliyochaguliwa ………. Mwaka wa masomo …………Shule nitokayo ……………….. Mahali ninapoishi …………….. Mkoa ………………… Anwani ……………….. Jina la Baba/Mlezi …………………………………Kazi yake ………………….. Wazazi/Walezi wanaishi wapi…………………pamoja/wametengana………………… Anwani ya mzazi/mlezi……………………… Simu …………………….. Wakati wa likizo nitakuwa kwa(mtaje) …………………………….. wapi……………. Nathibitisha kuwa taarifa hapa juu ni za kweli na sahihi Sahihi ………………………… Tarehe ………………….. KUKUBALI NAFASI Mimi ………………………………….nimesoma maagizo kwa makini na kuzielewa taratibu za shule na nipo tayari kuzifuata. Hivy nakubali nafasi niliyopewa na nitafika shuleni tarehe zilizopangwa.

B. IJAZWENA MZAZI/MLEZI

Mimi ………………………………………………ambaye ni …………….. wa mwanafunzi huyu nimesoma kwa makini maelekezo pamoja na sheria za shule.Nipo tayari ajiunge na shule hii, ninaahidi kumtolea ada, michango na mahitajiyote ili aweze kupata elimu yake vizuri. Aidha nitasaidiana na walezi wa shuleni katika kumlea mwanafunzi huyu katika maadili mema na kuitika wito wa kufika shuleni pale nitakapohitajika. Anwani yangu ya kudumu ……………………… Simu ………………………… Nikipata uhamisho ama kubadilisha makazi nitaijulisha shule kwa maandishi. Ndugu zangu wanaweza kumtembelea mwanafunzi akiwa shuleni siku za wageni ni;

1. …………………………..Uhusiano kwa mwanafunzi …………….. Simu …………
2. ……………………….…....Uhusiano kwa mwanafunzi …………….. Simu …………
3.… ……………………....Uhusiano kwa mwanafunzi …………….. Simu …………

Nathibitisha taarifa nilizotoa ni sahihi na kweli.

Sahihi ya mzazi/mlezi ……………………..…Tarehe……………….

**MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY IFUNDAGIRLS SECONDARY SCHOOL STUDENT'S MEDICAL CERTIFICATE**

To be completed by a Government Medical Officer and returned to the Headmistress of Ifunda Secondary School,P.O. Box7 Ifunda. To Medical Officer

………………………………………………………………………… …………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………

RE:STUDENT NAME………………………………………….. FORM……….COMB…………. AGE…….SEX………
Please,examine the student mentioned above and comment on her health by responding to the following items. Kindly put a tick or cross in front of eitherYes or No as you find appropriate. Thank you in advance. .................................... BLANDINA D NKONDOLA Do the student have problem in connection with • Sight? Yes/No If yes state………………………………………………………… …………………

•Hearing? Yes/No If yes state……………………….…………………………………..

• Speech? Yes/No If yes state……………………………………………………………….

• TB? Yes/No If yes state…………….…………………………………………………

• BloodPressure Yes/No If yes state…………………………..………………………………

• Any Physical disability? Yes/No If yes state…………………….………………………

Do you,therefore,recommend the said student medically fit for studentship at this school? Yes/No If no please state the reasons……………………………………………………………………………………

Name of Medical Officer……………………………..signature……………….

Designation & Stamp…………………………………Date………………………

**IFUNDA GIRLS SECONDARY SCHOOL**

**ORODHA YA VITABU KWA WANAFUNZI WA KIDATO CHA SITA NA TANO**

| | SOMO | JINA LA KITABU |
|---|---|---|
| | GENERAL STUDIES. | UNDERSTANDING GENERAL STUDIES FOR ADVANCED LEVEL BY JANNES BIGIRWAMUNGU.<br>GENERAL STUDIES FOR FORM 5 & 6 BY NYANGWINE<br>GENERAL STUDIES FOR FORM 6 BY RICHARD MBALASE<br>GENERAL STUDIES LIVE BY ZIST KAMILI |
| | GEOGRAPHY. | A COMPREHENSIVE APPROACH TRO PHYSICAL GEOGRAPHY BY MSABILA.<br>HUMAN AND ECONOMIC GEOGRAPHY BY MSABILA<br>PRACTICAL GEOGRAPHY ALIVE BY ZIST KAMILI |
| | HISTORY. | WOLD HISTORY BY IDRISA MSUYA<br>ADVANCED HISTORY PAPER 1 AND 2. BY SALEH YASSIN<br>LESSON NOTES FOR ADVANCED EDUCATION BY MWL BAKARI MADAYA |
| | KISWAHILI. | KISWAHILI 1.<br>NADHARIA YA LUGHA BY NYAMBARI NYANGWINE<br>KISWAHILI KIDATO CHA 5&6 BY TAI.<br>KISWAHILI 2.<br>NADHARIA YA FASIHI BY NYAMBARI NYANGWINE TAI.<br>TAHAKIKI YA KIDATO CHA 5 & 6 BY NYAMBARI NYANGWINE |
| | ECONOMICS. | ESSENTIALS FOR ECONOMICS(AMBROS)<br>ECONOMICS MADE SIMPLE(E.B.MWAKAGILE)<br>BASIC ECONOMICS (UGANDA)<br>ADVANCED ECONOMICS (TIE)<br>PRINCIPLES OF ECONOMICS.<br>DICTIONARY OF ECONOMICS. |
| | MATHEMATICS. | MAYOMBYA FORM 5&6 (CONCEPTUAL)<br>CHAND XI AND XII(MATHEMATICS ADVANCED)<br>SEPTINE I FORM 5&6 (TIE)<br>REVIEW PAPER 1&2 |
| | BIOLOGY. | FUNCTIONAL APPROACH.<br>UNDERSTANDING BIOLOGY.<br>BIOLOGICAL SCIENCE.<br>CONCERPTUAL BIOLOGY BY S.CHANDI.<br>BIOLOGY PRACTICALS BOOK.<br>TANZANIA INSTITUTE OF EDUCATION V AND VI. |
| | PHYSICS. | CHANDI XI AND XII ( PRINCIPLES OF PHYSICS)<br>ADVANCED PHYSICS FORM 5&6 BY TIE.<br>ABC MORDEN PHYSICS VOLUME I AND II. |

| | | |
|---|---|---|
| | | REVIEW PAPER 1 AND 2. |
| | CHEMISTRY. | PHYSICAL CHEMISTRY BY NGAIZA LUSIMA<br>GENERAL CHEMISTRY BY NGAIZA LUSIMA<br>INORGANIC CHEMISTRY BY NGAIZA LUSIMA<br>ORGANIC CHEMISTRY BY NGAIZA LUSIMA<br>SOIL AND ENVIRONMENTAL CHEMISTRY BY NGAIZA LUSIMA<br>CONCEPTUAL CHEMISTRY CHAND XI AND XII.<br>PHYSICAL,GENERAL,INORGANIC AND ORGANIC CHEMISTRY (TIE) |
| | ENGLISH. | ADVANCED LEVEL ENGLISH LANGUAGE 1 FORM 5&6 BY SHADRACK G NDAMBO AND JAMES IGNO KINUNDA<br>OXFORD LEARNERS DICTIONARY<br>ADVANCED ENGLISH LANGUAGE IN FORM 5&6 OXFORD<br>ADVANCED LEVEL LITERATURE THEORY AND ANALYSIS BY NICHOLOUS ASHELI<br>ADVANCED LEVEL LITERATURE BY NYAMBARI NYANGWINE |
| | BASIC APPLIED MATHEMATICS(BAM) | BASIC APPLIED MATHEMATICS TIE |